JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

Juni, 2023

Dodoma

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule: 0755668250**

**Makamu Mkuu wa Shule:0762125047**

**0767483941**

**Patron:0769300255**

**Shule ya Sekondari Matema Beach**

**S.L.P 122**

**10 Juni, 2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**…………………………………………….**
**S.L.P ……………………………………**
**……………………………………………**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATEMA BEACH HALMASHAURI YA KYELA MKOA WA MBEYA MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ………..

Shule ya Sekondari Matema Beach ipo umbali wa Kilometa 38 Kaskazini mwa Mji wa Kyela. Usafiri wa basi kutoka mjini Kyela unapatikana katika kituo cha mabasi Kyela Nauli ni Shilingi 3,000 kwa basi.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14**/08/2023**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13**/08/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/**08/2023**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni suruali mbili; (**Nyeusi** na **zambarau**)
**Suruali ishonwe kwa kawaida kabisa yenye mzunguko usiopungua inchi 14 miguuni kwa chini. Pia iwe na marinda ya mbele SIYO mitindo mingine ya kubana kama vile (MODO);**

ii. Mashati mawili meupe yenye mikono mirefu;

iii. Sare ya Michezo ni **viatu vya michezo, track suit na jezi ya blue** jozi moja;

iv. Viatu vya shule ni **vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi**

v. Soksi jozi mbili **nyeusi** za shule;

vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vii. Sweta nyeusi yenye shingo ya V;

viii. Nguo za kushindia (shamba dress) ni suruali ya rangi ya khaki;

ix. Tai mbili, moja nyeusi na nyingine ya zambarau;

x. Tisheti (T-shirt) aina ya form six (inapatikana shuleni);

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari makubwa angalau quire 3 counter books dazani moja;

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatishwa)

iv. Scientific Calculator kwa wanaosoma Hisabati na Jiografia ;

v. Godoro lenye urefu futi 6, upana futi 2.5 na unene angalau inchi 3.5

vi. Mashuka Jozi 2 rangi ya pinki, foronya ya godoro 1, chandarua 1;

vii. Nguo za ndani za kutosha;

viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) au Moja ya Lita 20; zenye mifuniko;

x. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

### 2.3 Michango mbalimbali

a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**MUHIMU: Michango ilipwe kupitia benki kwenye akaunti ya shule namba 60901200054.**
**Jina la akaunti ni Matema Beach Secondary School.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule na mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHU<u>LE</u> HII**




**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). **Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-**

- **Mkuu wa shule 0755668250**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0762125047 / 0767483941**
- **Mwandamizi Taaluma 0752660902**
- **Mwandamizi Malezi 0756520265 / 0621050687**

**FOMU A**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**(THIS FORM IS TO BE COMPLETED BY A MEDICAL OFFICER).**

Name of pupil ……………………………………………………………………………………. Age …………………………………………………. Sex ……………………………………….. The above named has been examined in respect of

(a) STOOL ……………………………………………………………………………

(b) URINE ……………………………………………………………………………..

(c) CHEST ……………………………………………………………………………

(d) BLOOD …………………………………………………………………………….

(e) EYES ……………………………………………………………………………….

(f) EARS …………………………………………………………………………………

(g) OTHER FINDINGS ……………………………………………………………….…...

……………………………………………………………………….

……………………………………………………………………..…

…………………………………………………………………………

I am satisfied that the above named pupil is /is not fit to pursue further studies in any secondary school.

…………………………

SIGNATURE

………………………………

DATE

…………………………

DESIGNATION

……………………………..

STATION

**FOMU B**

**MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

**(IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE)**

Mimi (taja jina lako kamili) ………………………………………………………….. nimechaguliwa kujiunga na masomo ya Elimu ya Sekondari kidato cha V **2023** katika Shule ya Sekondari Matema Beach. Najaza fomu hii kukubaliku chaguliwa kwangu kuendelea na masomo katika shule hii. Naahidi kuwani wapo katika shule hii nitatii na kufuata sheria na kanuni zote za shule kwa kipindi chote cha masomo yangu.

Pia na ahidi kuwa kwa muda wote ni wapo katika shule hii sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Kama nitakiuka na kwenda tofauti na mkataba huu, naomba sheria kali zichukuliwe dhidi yangu yaani **kufukuzwa shuleni** na **kushtakiwa Mahakamani**

Nakubali kuwa nimesoma na kuelewa yote katika fomu hii ya mkataba na ninaahidi kuwa nitatekeleza na kufuata sheria na kanuni zote za shule.

**SAHIHI YA MWANAFUNZI** …………………………………….

**TAREHE** ……………….……………………

## FOMU C

## FOMU YA MZAZI / MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI, KULIPA ADA, MICHANGO NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE

### (IJAZWE NA MZAZI / MLEZI MWENYEWE)

Mimi mzazi / mlezi (Jina kamili ………………………………………………………… Ambaye ni mzazi / mlezi wa (Jina kamili la mwanafunzi) ……………………………………………… najaza fomu hii kukubali maelezo yaliyoandikwa hapo juu. Kwa kujaza fomu hii. Naahidi kuwa nitatekeleza kwa vitendo katika kuhakikisha kuwa mwanafunzi huyu anapata mahitaji yote (yake binafsi na mahitaji ya shule) kwa muda wake wote wa masomo ya Elimu ya Sekondari akiwa Matema Beach Sekondari.

Iwapo sitatimiza wajibu wangu, naahidi kuwa sheria zichukuliwe dhidi yangu.

**SAHIHI YA MZAZI / MLEZI** ………………………………………

**TAREHE** ……………………………………

**FOMU D**

**HABARI KUHUSU MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi (Jina hili ndilo litakalotumika siku zote bila kubadilika)

   …………………………………………………………………………………………….

2. Tarehe ya kuzaliwa: ……………………………………………………………………………

3. Mahali alipozaliwa (Wilaya): …………………………………………………………………….

4. Mahali anapoishi sasa (Wilaya): …………………………………………………………….

5. Jina la Baba / Mlezi: ……………………………………………………………………………

6. Anuani ya Baba / Mlezi: ……………………………………………………………………….

   …………………………………………………………………………..

7. Namba ya simu........................................................., ...........................................................

8. Jina la Mama / Mlezi: ……………………………………………………………………………

9. Dini ya Mwanafunzi: ……………………………………………………………………………

10. Dini ya Baba / Mlezi: …………………………………………………………………………..

11. Dini ya Mama / Mlezi: …………………………………………………………………………..

12. Kazi ya Baba / Mlezi: ………………………………………………………………………….

13. Michezo atakayoshiriki shuleni ni: ………………………………………………………….

    …………………………………………………………………………………………………

    ………………………………………………………………………………………………..

**FOMU E**

**MKATABA WA KUDHIBITI MAJANGA YA MOTO NA MATUMIZI YA SIMU KWA WANAFUNZI**

**(IJAZWE NA MWANAFUNZI PAMOJA NA MZAZI)**

Mimi (taja jina lako kamili)______________________________________________nimechaguliwa kujiunga / Mwanafunzi wa kidato cha___________mwaka ______________

Ninaahidi kuwa niwapo katika shule hii sitatumia au kumiliki simu . Kama nitakiuka au kwenda kinyume na mkataba huu nitakuwa tayari kuadhibiwa kulingana na sheria ya shule inayopiga marufuku matumizi ya simu na adhabu yake ni **kufukuzwa shule au kulipa fidia isiyopungua 800,000/= (Mia Nane Elfu tu)** kwa kosa la matumizi ya simu na kuhatarisha usalama . Endapo kuna uharibifu wa miundombinu ya shule adhabu itatolewa baada ya tathmini ya Bodi ya shule. Adhabu hiyo inaweza kuongezeka au sheria ya makosa ya jinai kutumika.

SAHIHI YA MWANAFUNZI TAREHE

____________________ __________________

Mimi______________________________________ambaye ni mzazi/ mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa katika mkataba huu nimesoma na kuelewa na nitakuwa tayari kuwajibishwa kulingana na mkataba huu.

SAHIHI YA MZAZI/ MLEZI ____________________ TAREHE____________

SIMU YA MZAZI/MLEZI _____________________

**FOMU F**
**ORODHA YA VITABU MUHIMU VYA KIADA, ZIADA NA REJEA:**

**MWANAUNZI ANASHAURIWA KUTAFUTA VITABU VYA KIADA HUSUSANI VINAYOTOLEWA NA TAASISI YA ELIMU TANZANIA (TET/TIE)** NA VITABU VYA **ZIADA** NA **REJEA** AMBAVYO MWANAFUNZI ANAWEZA KUTAFUTA AU KUNUNUA KWA AJILI YA KUJISOMEA KUTEGEMEANA NA TAHASUSI ALIYOCHAGULIWA.

**A. HISTORY**

1. Learning Advanced World History Book Two for Advanced SS- IDRISSA R MSUYA
2. Learning Advanced Africa History Book One for Advanced SS- IDRISSA R MSUYA
3. Major Issues in Africa History ICD
4. Major Events in Africa History MWIJAGE
5. The Political Economy Emperialism NABUDERE
6. Africa Since 1800 4th Edition Roland Oliver Atmore
7. The Making of Modern Africa Vol 1
8. How Europe Underdeveloped Africa WALTER RODNEY
9. The 20th Century DUFF M. N
10. Europe from 1815 PEACOCK
11. By Webster J.B. The Growth of African Civilization, the Revolutionary Years ofWest Africa Since 1800, Longman Press.

**B. GEOGRAPHY**

1. Certificate of Geography (Oxford for Three by Mary Mugo, Robert Kuragga and Paul Kibuuka
2. General Geography in Diagrams Rb Bunnet
3. Photography Interpretation and Elementary Surveying for Secondary Level New Edition S. E. Dura
4. Regional Geography Nyangwine/ Msabila
5. Certificate Human and Economic Geography Morgans and Leong Chang
6. Principles in Physical Geography Monkhouse
7. Geography an Integrate Approach David Waugh (2014)
8. Dictionary of Geography Dr. R. M. LODHA

**C. ENGLISH LANGUAGE**

**PAPER 1**

1. A COMPLETE ENGLISH Course For Form Six Michael Kadeghe
2. English For Form Five And Six Michael Kadeghe
3. Teaching English As A Foreign Language G. Broughton, Et Al
4. Longman English Grammar L. G. Alexander
5. Advance Learners Dictionary Oxford
6. Advanced Level English Language Nicholous Asheri
7. Nichlolus Arshery, Comprehensive English Grammar New edition.
8. Michael Kadeghe, Semantics Phonology and Stylistics (blue)

**PAPER 2**

**1. NOVELS**

a) The Beautiful Ones are not yet Born — A. K. Amah
b) A Grain of Wheat — Ngugi wa Thiong'o
c) A Man of the People — Chinua Achebe
d) Vanishing Shadows — N. Kayombo
e) His Excellency the Head of State — Dany Safo

**2. POETRY**

a) Selected Poems From Taninstitute of education
b) The Wonderful Surgeon — Charles Mloka

**3. PLAYS**

a) I Will Marry when I Want — Ngugi wa Thiong'o And Ngugi wa Mirii
b) Betrayal in the City — Francis Imbuga
c) An Enemy of The People — Henrik Ibsen

## D. KISWAHILI

**1. SARUFI**

a) SAMIKISA — D. P MSAMBA
b) SAMAKISA — D. P MSAMBA
c) FASIHI — F. SENKORO
d) Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo — F. NKWERA
e) Kitangulizi cha Tafsiri — Mwansoko
f) Kamusi ya Kiswahili Sanifu — BAKITA
g) Tahakiki kidato cha tano na sita.
h) Nadharia ya Fasihi kidato cha tano na sita Kiswahili II.
i) Kiswahili – I: Mwandishi Masuko Christopher Saluhaya.

**2. USHAIRI**

a) KIMBUNGA — G. GORA (TUKI)1994
b) Mapenzi Bora — S. ROBERT
c) Chungu Tamu — T. Mvungi
d) Fungate ya Uhuru — M. S. Khatib

**3. RIWAYA**

a) Vuta Nkuvute — Shafi A. Shafi
b) Usiku Takapokwisha — Mbunda
c) Kufikirika — S. Robert
d) Mfadhili — Hussein Tuwa

**4. TAMTHILIA**

a) Kivuli Kinaishi — S. Mohamed
b) Morani — E. Mbogo
c) Kwenye Ukingo wa Thim — I. Hussein
d) Nguzo Mama — Penina Muhando

## E. MATHEMATICS

### 1. ADVANCED MATHEMATICS

a) Pure Mathematics I & II — J. K. Backhouse
b) Pure Mathematics — C. J. Trunter
c) Advanced Mathematics — S. Chandler & L. Bostock
d) Understanding Mathematics — A. J. Sadler
e) Core Mathematics for Advanced Level — S. Chandler & L. Bostock
f) S. Chands Mathematics for Class XI & XII — H. K. Dass

### 2. BASIC APPLIED MATHEMATICS

a) Basic Applied Mathematics for advanced level Form V&VI — TIE

## F. ECONOMICS

1. C.M. Ambilikile – Advanced level paper two and professional studies
2. Economic 2; Advanced levels paper two and professional studies
3. Economic simplified (revised and update)
4. Undestanding Economics (Remed H. Chegee.M)
5. Modern Economics — Mudida
6. Managerial Economics — Oxford
7. Micro Economics — Meconnel Brue
8. Micro Economics — TIE
9. Macro Economics — TIE

## G. GENERAL STUDIES

1. General Studies Approach.
2. General Studies for Advanced Level — Joaness Bogirwamungu, Sospeter M. Deogratias